# SUA: Ufugaji sungura una faida nyingi, lakini wananchi hawafahamu

*Na Christina Cosmas*

UFUGAJI wa sungura umekuwa na faida nyingi bila watu kujua duniani na hivyo kubaki wakifuga wanyama wengine.

Afisa Mifugo Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Hyasinta Minde, anaeleza faida za ufugaji wa sungura kama wanyama wanaoweza kusogeza mbele mnyororo wa thamani na kuongeza vipato vya wafugaji, akisema kwamba licha ya mauzo ya wanyama hao kuwa ni ya bei juu, lakini pia mfugaji anaweza kunufaika kwa kuuza mkojo kama dawa ya kuua wadudu kwenye mboga na matunda.

Minde anasema licha ya faida ya nyingine ya kufuga sungura kuwa ni nyama lakini mfugaji anaweza kufuga sungura wengi apendavyo na kuweka vifaa vya kutegea mkojo ambao atauhifadhi kwa usafi na baadae kupaki kwenye chupa na kuweza kuuza kwa wakulima au kufanya matumizi ya kilimo yeye mweneywe.

Anasema, lita moja ya mkojo wa sungura huuzwa kwa shilingi 10,000 za kitanzania ambapo akiwa na sungura wapatao 20-30 anaweza akakusanya mkojo ndani ya miezi 6 anaweza kupata lita 12 na kuuza kwa wakulima na kujipatia sh. 120,000 na kukuza uchumi wake na taifa kwa ujumla huku akifikia uchumi wa kati unaokusudiwa kwa sasa.

Hyasinta anasema pia kinyesi cha mnyama sungura kinaweza kuwa biashara nzuri kwa mfugaji pia kufuatia kuuzwa kwa shilingi 250 za kitanzania kwa kilo 10 za kinyesi cha sungura.

Anasema, sungura mmoja anaweza kuuzwa kwa kiasi cha shilingi inategemea na mahali anapouzwa au alipofugwa sambamba na ubora wake.

Kwamba, zipo aina nyingi za sungura ikiwemo California white, German Giants, Newsland White, American Sports, Angola, kutch na chinchilla ambao wanapatikana SUA kwa sasa.

Afisa huyo anasema sungura mmoja anabeba mimba kwa siku 8-35 wastani wa mwezi mmoja na anaweza kuzaa watoto wasiopungua 8-12 kwa uzao mmoja ambapo kwa ufugaji uliobora anaweza kuzaa mara 5 kwa mwaka na hivyo mfugaji kuwa na wastani wa sungura 40.

Anasema ipo faida kubwa katika ufugaji wa wanayama hao kutokana na kwamba hawampi mfugaji mawazo kufuatia kula pumba tu na maji na kuendelea kukua.

Hyasinta anasema ufugaji wa sungura hadi kukua unachukua miezi 8-12 na kuwa tayari kwa kuliwa iwe kwa sungura wa kizungu 'broiler' au wa kienyeji.

Anasema nyama ya sungura inafanana na nyama ya kuku ambayo ni sehemu ya nyama nyeupe inayofaa kuliwa na kila mtu na kumuongezea protini mwilini.

Hyasinta anasema sungura anatakiwa kuepushwa na majimaji wakati anapofugwa, ambapo mabanda yao yanapaswa kuwa juu juu na kuwa na sehemu ya chini ya kushusha mkojo na kinyesi.

Anasema zipo changamoto zinazompata mnyama Sungura wakati wa ufugwaji ambao ni pamoja na magonjwa ya kuhara damu na minyoo ya ngozi ambayo kwa ujumla yanatibika katika Hospitali ya Rufaa ya Wanyama SUA, hospitali nyingine za wanyama na kutumia dawa kutoka kwa maduka ya dawa za mifugo yanayotambulika.

Hata hivyo, anasema mkojo wa sungura kama dawa ya kuua vijidudu waharibifu wa mboga na matunda hauleti madhala kama mtumiaji atatumia kwa kufuata ushauri anaopewa.

Hivyo aliwataka wakulima na wafugaji kutembelea banda la maonesho ya wakulima la SUA lililopo kwenye sherehe za wakulima Kanda ya Mashariki kupata elimu juu ya ufugaji wa sungura kwa faida na elimu zingine.

Dkt Isaack Kashoma ambaye ni Daktari Mkuu Hospitali ya Wanyama SUA, anasema SUA wanahospitali kubwa maalum kwa ajili huduma kwa wanyama wote ambayo wanyama wanaofugwa na wasiofugwa (wanyamapori) kwa huduma za kupima na ugunduzi wa magonjwa yanayosumbua wanyama, matibabu, chanjo na ushauri.

Anasema hospitali ya wanyama SUA ni hospitali pekee ya rufaa ya kwanza ya wanyama kwa Tanzania ilianzishwa mwaka 1984 wakati chuo kinaanzishwa na kuboreshwa zaidi kuwa na vifaa maalum kuanzia mwaka 2015 na inaendelea kuboreshwa kwa sasa, ili kila kitu kinachotakiwa kwa ajili ya ugunduzi wa magonjwa kwa wanyama kiwepo.

Dkt Kashoma anasema kwa mnyama kama Sungura, nguruwe, ngamia, na wengine wanawahudumia kitiba pale wanapokuwa na magonjwa.

Anasema kuna chanjo za kishaa cha mbwa wanaendelea kutoa kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya magonjwa mbalimbali yakiwemo ya kuharisha, na kutapika na homa ya manjano ambapo kwa wiki wastani wa mbwa 50 wanapata chanjo katika magonjwa hayo kutoka Mkoa wa Morogoro.

Aidha, anasema pia wamekuwa wakitoa huduma kwa wagonjwa kutoka mikoa mbalimbali ikiwemo Dar es salaam, Tanga, Dodoma, Iringa na Pwani kwa huduma za mbwa wanaopelekwa kwa rufaa wakiwemo waliovunjika sehemu na kuwa na uhitaji wa kuungwa, wanauvimbe sehemu, wenye uhitaji wa x-ray ambapo matibabu yake hutolewa hospitalini hapo na kuondoka wakiwa na afya njema.

Awashauri wakulima kutambua kwamba ufugaji wanyama mbalimbali una faida kubwa hivyo wajenge dhana ya kuwapenda wanyama wao na wasisite kuwapelekea hospitalini SUA wanapoumwa kwani gharama za matibabu ni nafuu sana.

Amewataka wakulima watembelee banda la SUA kupata ushauri wa masuala mbalimbali ya mifugo, ambako kwa kipindi hiki cha 88 wanatoa huduma za chanjo ya kichaa cha mbwa bure, hivyo wakulima hawana budi kwenda kupata huduma hiyo na nyinginezo.

Hata hivyo, anasema changamoto wanayoipata ni kuwafikia wanyama pori kwa matibabu ambapo anasema, endapo miundombinu au njia maalum ya kuwafikia baadhi ya wanyama, hasa wakali itakapoandaliwa vizuri wanaweza kuwapata kwa wakati na kuwahudumia vyema na hivyo kuendelea kukuza rasilimali za taifa.



Scanned with CamScanner

MAAGIZO

# Waziri aagiza kuku kuuzwa kwa kilo

Herieth Makwetta, Mwananchi
hmakweta@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewataka wafugaji wote wa kuku wa nyama nchini kuanza kuwauza kwa kilo.

Kwa kipindi kirefu wafugaji wamekuwa wakiuza kuku wa nyama kwa Sh5200 kwa walanguzi ambao mara nyingi wao sokoni huuza kwa bei ya Sh6500 hadi Sh8000 ilhali kuku hao huwa na uzito wa kilogramu 1.5 mpaka 2.5.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana alipokuwa akisikiliza kero za wafugaji wa kuku.

"Ninawaagiza wafugaji wote kuanzia leo anzeni kuuza kuku wenu kwa kilo na achaneni na mazoea ya bei za kukadiria," alisema na kuongeza:

"Sitatoa bei elekezi kwani itaamuliwa na soko, lakini atakayeuza kwa kusukuma tu atashughulikiwa," alisema.

Awali wakitoa kero zao, wafugaji hao walilalamikia ughali wa bei za vifaranga pamoja na chakula, huku uuzaji wa kuku walio tayari ukiwa chini na kuwasababishia hasara.

Mmoja wa wafugaji hao Mashaka Puya alisema wanunuzi wa kuku wamekuwa na kawaida ya kuchunguza kwa macho pindi wanapotaka kununua kuku kwa kupima mwonekano wa kidari.

"Hatuna masoko, tunasubiri wafugaji waje wanunulie majumbani na hilo linatuumiza sana. Anakuja mnunuzi ananyanyua kuku, anatazama kidari, anakukadiria kuku wako nitanunua kwa Sh5200' wengine mpaka Sh4,800," alisema Puya.

**MIZANI**



"Tuacheni upangaji wa bei ya kuku kwa macho, kuanzia sasa tutaweka mizani maeneo kadhaa ndani ya jiji ala Dar es Salaam ili tuuze kwa kilo"
**Mashimba Ndaki**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## Tume ya Haki za

hazitapatiwa ufumbuzi zitawa-
rudisha nyuma.

HABARI LEO UK 17.



# Ndaki: Marufuku kuuza kuku eneo la Tazara Dar

**Na Oscar Job**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amepiga marufu uuzaji wa kuku eneo la Tazara na kuziagiza kamati za ulinzi na usalama za wilaya za Temeke na Ilala kuwachukulia hatua haraka wale wote watakaobainika.

Pia, ameonya kuhusu tabia za wazalishaji wa vifaranga na chakula kuku, kuwawekea masharti yasiyo na msingi wafugaji wa kuku, kwa lengo la kuvutia biashara.

Badala yake, amewataka wazalishaji hao kushindana wao kwa wao ili kuwavutia wafugaji.

Alisema hayo katika mkutano wa wazi wa wazalishaji na wafugaji wa kuku wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani jana.

Waziri Ndaki alisema kwa kipindi kirefu sekta ya ufugaji wa kuku, imekuwa ikichezewa na hivyo kuwaathiri wafugaji.

Alisema kitendo cha baadhi wafanyabiashara hususani wazalishaji wa vifaranga na vyakula vya kuku, kuligeuza eneo la Tazara kama mnada wa kuuzia kitoweo hicho kifikie mwisho, kwa kuwa siyo eneo linalotambuliwa kisheria.

"Kuanzia leo naomba iwe mwanzo na mwisho biashara ya kuku kufanyika katika eneo la Tazara, kamati za ulinzi na usalama zinazohusika na eneo hilo zianze kufuatilia kuanzia sasa na kuwachukulia hatua wahusika" alisema Ndaki.

Scanned with CamScanner

NIPASHE UK 16

# Wafugaji Mbarali waelewa suluhu migogoro ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAFUGAJI wa Wilaya ya Mbarali, wameshauriwa kununua ardhi kwa ajili ya kuchungia mifugo yao badala ya kutegemea maeneo yaliyotengwa na serikali ili kuondokana na migogoro ya ardhi ambayo imekuwa ikiibuka mara kwa mara.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya hiyo, Reuben Mfune, alisema wakati akizungumza na Nipashe na kutumia nafasi hiyo, kuwataka wafugaji kuacha tabia ya kuingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima na kwenye Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ili kuepusha migogoro, ambayo husababisha mapigano ya mara kwa mara.

Alisema maeneo yaliyotengwa na serikali hayatoshi kwa ajili ya matumizi ya wafugaji na wakulima, hivyo kufanya maeneo yaliyotengwa na Serikali na makazi ya watu kuvamiwa.

"Mfugaji ambaye umeamua kufuga mifugo mingi unatakiwa ununue ardhi yako na hiyo itasaidia kuhifadhi na kutunza mazingira kwa sababu kila mmoja atakuwa na uchungu, sitakubali kuona maeneo yaliyotengwa na serikali yanaharibiwa kwa ajili ya shughuli za kilimo na mifugo," alisema Mfune.

Baadhi ya wafugaji walimweleza Mfune matatizo yanayowakabili ikiwamo uhaba wa maeneo ya kuchungia huku wakiomba serikali kulifuta Tangazo lake namba 28 la mwaka 2008 (GN 28) ambalo lilipanua Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, hivyo kupunguza maeneo ya kuchungia.

Mmoja wa wafugaji hao, Shaban Olelengananu, ambaye ni mfugaji wa Kijiji cha Mwanavala, alisema Kijiji hicho kina eneo la wafugaji ambalo lilipimwa wakati wa uwekaji wa matumizi bora ya ardhi, lakini limevamiwa na wakulima.

Alisema hali hiyo imewafanya wafugaji kukosa maeneo ya kuchungia na kwamba wakitaka kuchungia katika eneo hilo inaibuka migogoro na wakulima ambao alidai ndio wavamizi.

"Sisi wafugaji tunakuwa kama hatuhitajiki katika Wilaya hii, watu wa Tanapa wanatuzuia kuchungia kwenye hifadhi, wakulima nao wamevamia eneo letu lakini hakuna hatua zilizochukuliwa na Serikali," alisema Olelengananu.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali, Hashim Mwaliaga, alimuomba Mkuu wa Mkoa kusaidia kufikisha kilio cha wananchi wa wilaya hiyo ili mipaka ya hifadhi irekebishwe.

Alisema GN 28 ndio chanzo kikubwa cha migogoro ya ardhi katika wilaya hiyo kwa maelezo kuwa imechukua maeneo mengi ya wananchi wilayani humo na kuyafanya kuwa sehemu ya hifadhi.